

**SHULE YA UPILI YA GATITU S.L.P. 010310 327 GATUNDU**  
**MTIHANI WA KATI YA MUHULA WA PILI**  
**KIDATO CHA PILI 2016**

jina.....nambari.....darasa.....

jibu maswali yote

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuatia.

**SIWANIE UKUU.**

Sioni ulichoshika, upande ule na huu,  
Sipokuwa kuzunguka, ukitafuta ukuu,  
Ni mkuu unasaka, utavunjika maguu,  
Siwani kwenda juu, hata chini hujafika.

Mpanda ngazi hushuka, kumbuka usemi huu,  
Na pengine huanguka, usibukue nafuu,  
Mbonawe hujazinduka, mchana mashekuu,  
Siwani kwenda juu, hata chini hujafika.

Umaarufu wataka, ili uwe juu juu,  
Bali nikikumulika, hukwei hata chuguu,  
Kwenye ngazi taanguka, kwa kishindo chini puu,  
Siwani kwenda juu, hata chini hujafika.

Ungetaka faidika, ujaze lako bunguu,  
Usiende kwa haraka, papara zina makuu,  
Chembechembe huumuka, huleta tija shafuu,  
Siwani kwenda juu, hata chini hujafika.

a. Shairi hili ni la aina gani? Kwa nini?

(alama2)

.....  
.....

b. Muundo wa shairi hili ni upi?

(alama 6)

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

c. Taja utao wa mleo wa ubeti wa tatu

(alama1)

.....

e. Andika mfano mmoja wa uhuru wa mshairi kama ulivyotumiwa na mshairi katika hairi hili.

(alama2)

.....

.....

f. Shairi hili ni la arudhi. Thibitisha.

(alama2)

.....

.....

g. Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi.

i. Unasaka.

(alama1)

.....

ii. Huumuka.

(alama1)

.....

### **MATUMIZI YA LUGHA**

1. Andika sentensi ifiatayo katika usemi wa taarifa.

(alama3)

"Itabidi tukutane kesho ili tutafute namna ya kutatua tatizo hili linalotishia mifugo wetu," Mzee Bakari akaambia wanakijiji.

.....

.....

2. Kwa kutunga sentensi **onyesha** tofauti ya **vitate** hivi.

(alama 2)

(i) Pua na bua

.....

.....

3. Andika sentensi ifuatayo upya ukitumia hali ya **-ngali-**.  
Ukikesha utasinzia darasani

(alama 2)

.....

4. Eleza matumizi moja moja ya **viwakifishi** vifuatavyo:

(alama 3)

(i) Kistari kirefu.

.....

(ii) Mshazari.

(i) Parandesi.

5. Geuza sentensi hii iwe katika **kauli ya kutendesha**. (alama 2)  
Mama humfanya mtoto wake kula.

6. Tambua aina za vitenzi katika sentensi,  
Hawa sio wachezaji waliokuwa wakicheza jana (alama3)

7. Andika katika ukubwa (alama 2)  
Mke wa mzee huyu hupenda watoto sana.

8. Andika katika hali ya mazoea kwa kutumia kirejeshi 'o'  
Mtoto ambaye hula lishe bora ndiye hukua nyema. (alama 2)

9. Tambua hali na wakati gani katika sentensi ifuatayo:  
Zawadi atakuwa anasoma nitakapofika. (alama 2)

10. Yakinisha sentensi ifuatayo katika wingi. (alama.2)  
Serikali isingelela msaada wa chakula wananchi wasingenusurika.

11. Tumia kivumishi cha pekee katika sentensi kuonyesha :

(i) Umilikaji (alama 2)

(ii) Ziada

### **ISIMUJAMII**

nitakupa ... viuavinja ambayo utatumia kwa siku tano. Asubuhi moja na kabla ya kulala. Tumia maji mengi unapoimeza. Utaona sista hapo nje na atakupatia appointment... Hakikisha kuwa hutatumia vileo hadi ukamilishe ...

a) Taja sajili inayolejelewa na maneno haya. (alama2)

b) Kwa kutumia kifungu hiki, eleza sifa nne muhimu zinazohusiana na sajili uliotaja hapo juu. (alama8)

.....  
.....  
.....  
.....

**FASIHI SIMULIZI (alama10)**

a) Eleza maana ya misimu.

(alama 2)

.....  
.....

b) Eleza sifa nne za misimu.

(alama 4)

.....  
.....  
.....  
.....

c) Nyiso ni nini ?

(alama1)

.....

d) Fafanua sifa zozote tatu za nyiso

(alama3)

.....  
.....  
.....  
.....  
.....